MWONGOZO WA ELIMU YA FEDHA

KWA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU NA KATI

2026

YALIYOMO

1.0 Utanguli 1

1.1 Malengo ya Mwongozo 1

2.0 Mada 2

2.1 Kupanga Bajeti 2

2.1.1 Hatua za Kuandaa Bajeti Yako 3

2.1.2 Mfumo wa Kupanga Bajeti 3

2.1.3 Athari za kutokuwa na bajeti 5

2.2 Akiba 7

2.2.1 Akiba ya Dharura 7

2.2.2 Akiba ya Maendeleo 7

2.2.3 Mambo Ya Kuzingatia Ili Kuweka Akiba 8

2.2.4 Umuhimu wa Akiba 8

2.2.5 Changamoto za Kutokuweka Akiba 9

2.2.6 Hitimisho 9

2.3 Uwekezaji 12

2.3.1 Dhana Muhimu Kuhusu Uwekezaji 12

2.3.2 Baadhi ya Aina za Uwekezaji 13

2.3.3 Hatua Salama za Kuanza Uwekezaji 14

2.3.4 Hitimisho 15

2.4 Kukopa kwa Hekima 17

2.4.1 Mambo Muhimu ya Kuzingatia Kabla ya Kukopa 17

2.4.2 Jinsi ya Kutambua Mkopo Salama 18

2.4.3 Kituo cha Taarifa za Mikopo (Credit Reference Bureau) 18

2.4.4 Ujumbe Muhimu Kuhusu Mkopo wa HESLB..... 19

2.4.5 Mambo ya Kuzingatia 19

2.5 Kujilinda Dhidi ya Utapeli wa Kifedha na Upatu Haramu 21

2.5.1 Sifa Kuu za Utapeli wa Kifedha 21

2.5.2 Aina za Utapeli wa Kifedha Kidijitali 22

2.5.3 Namna ya Kujilinda Dhidi ya Utapeli wa Kifedha 24

2.5.4 Madhara ya Utapeli wa Kifedha 24

2.5.5 Kuripoti Utapeli wa Kifedha 25

2.5.6 Hitimisho 25
2.6 Jihadhari na Upatu 27
2.6.1 Maana ya Upatu 27
2.6.2 Kiini cha Tatizo 27
2.6.3 Tofauti Kati ya Upatu na Uwekezaji 28
2.6.4 Aina na Upatu 29
2.6.5 Madhara ya Kushiriki Upatu 30
2.6.6 Taarifa na Kupata Msaada 31
2.6.7 Hatua za Kujilinda na Upatu 31
2.6.8 Hitimisho 31
2.7 Kipato 33
2.7.1 Faida za kuwa na Kipato 33
2.7.2 Vyanzo Vya Kipato (Fedha) Kwa Mwanafunzi 33
2.7.3 Faida na Hasara za Vyanzo mbalimbali vya Kipato (Fedha) 34
2.7.4 Njia za Kufanya Biashara 36
2.7.5 Hitimisho 37
2.8 Kujitegemea 39
2.8.1 Faida na Hasara za Njia za Kijiajiri na Kuajiriwa 40
2.8.2 Namna ya Kujilinda na Hasara za Kuajiriwa na Kujiajiri 41
2.8.3 Hitimisho 42
3 Marejeo 44

1.0 Utangulizi



Elimu ya fedha ni maarifa muhimu yanayomwezesha mtu kupanga, kusimamia na kutumia fedha zake kwa ufanisi ili kufikia malengo yake ya kifedha. Elimu hii ni muhimu kwa mwanachuo kwa kuwa humsaidia kusimamia fedha anazopata kutoka Bya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), wazazi, walezi, ufadhili au shughuli za kujiongezea kipato. Kupitia mwongozo huu mwanafunzi atajifunza kupanga bajeti, kutofautisha mahitaji ya muhimu na ya hiari, kuweka akiba, kuepuka matumizi yasiyo ya lazima na kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya fedha, uwekezaji na ujasiriamali. Maarifa haya yatamsaidia mwanafunzi kujengea tabia nzuri za kifedha, kujitegemea, kuwa na utulivu wa kifedha hivyo kuongeza uwezekano wa kufanikisha malengo yake ya kitaaluma na maisha kwa ujumla.

1.1 Malengo Ya Mwongozo

Lengo Kuu la mwongozo huu ni kuwawezesha wanafunzi wa vyuo vikuu na vyuo vya kati kupata maarifa, ujuzi na mtazamo sahihi kuhusu usimamizi wa fedha binafsi kama vile kupanga bajeti, kuweka akiba, kufanya maamuzi sahihi kuhusu mikopo, na kujenga tabia bora za kifedha.

Baada ya kusoma mwongozo huu, mwanafunzi anatarajiwa kuwa na uwezo wa:

i. Kueleza umuhimu wa elimu ya fedha katika maisha ya mwanafunzi wa chuo;

ii. Kuandaa na kusimamia bajeti binafsi kwa kuzingatia mapato, matumizi, akiba na vipaumbele vya kifedha;

iii. Kutofautisha kati ya mahitaji ya msingi na matamanio ili kufanya matumizi sahihi ya fedha;

iv. Kutumia fedha kwa nidhamu kwa ajili ya kufikia malengo ya muda mfupi na muda mrefu;

v. Kutathmini fursa za mikopo kwa kuelewa gharama, masharti na uwezo wa kurejesha kabla ya kukopa;

vi. Kutambua umuhimu wa kurejesha mikopo kwa wakati na kujenga historia nzuri ya ukopaji; na

vii. Kutumia maarifa ya kifedha kujenga msingi imara wa kujitegemea

kiuchumi, uwekezaji na ustawi wa kifedha baada ya kuhitimu masomo.

2.0 Mada



Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia mazingira halisi ya maisha ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaopokea fedha za kujikimu kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB). Maudhui yake yamejikita katika mada kuu saba zinazolenga kuwajengea wanafunzi uelewa na ujuzi wa kusimamia fedha kwa ufanisi pamoja na kufanya maamuzi sahihi ya kifedha katika kipindi chao cha masomo. Mada hizo ni :

i. Kupanga Bajeti
ii. Akiba
iii. Uwekezaji
iv. Kukopa kwa Hekima
v. Kujilinda Dhidi ya Utapeli wa Kifedha
vi. Kipato halali
vii. Kujitegemea

2.1 Kupanga Bajeti

Bajeti ni makadirio ya jinsi utakavyotumia fedha zako kabla hujaanza kuzitumia. Kwa maneno mengine, bajeti ni mwongozo unaokusaidia kuelekeza fedha zako kwenye mahitaji muhimu na kukuepusha na matumizi yasiyo ya lazima.

Je, umewahi kujiuliza kwa nini wanafunzi wawili wanaopata kiasi sawa cha fedha za kujikimu wanaweza kuwa na matokeo ya kifedha tofauti kabisa? Mmoja huishiwa na fedha za kujikimu mapema na kuanza kukopa, wakati mwingine fedha humtosha hadi mwisho wa muhula.Tofauti hiyo haisababishwi na kiasi cha fedha walichopata, bali Matumizi ya fedha hizo.

Kwa lugha rahisi, bajeti ni ramani ya matumizi ya fedha zako. Kama vile msafiri anavyohitaji ramani ili afike anapokwenda bila kupotea, ndivyo fedha zako zinavyohitaji bajeti ili zisitumike hovyo na kuisha kabla ya wakati.

> **Kumbuka:** ***Usipopanga matumizi yako, fedha zako zitakupangia maisha yako.***

2.1.1 Hatua za Kuandaa Bajeti Yako

1. **Orodhesha fedha zako zote:** Mkopo wa HESLB, pesa kutoka kwa wazazi, kipato cha kazi ndogo, zawadi n.k;
2. **Orodhesha matumizi yako yote:** Chakula, malazi, nauli, vitabu, internet, simu n.k;
3. **Toa matumizi kutoka kwenye fedha zako:** Kama fedha zako zinazidi matumizi ina maana uko vizuri! Kama matumizi yanazidi fedha zako ina maana hauko vizuri kwenye matumizi yako hivyo punguza haraka matumizi yasiyo ya lazima;
4. **Weka akiba kwanza:** Kabla ya kutumia chochote, tenga 15% ya fedha zako zote kwenye akaunti tofauti; na
5. **Fuatilia bajeti kila wiki**: Angalia kiasi kilichosalia baada ya matumizi angalau mara moja kila wiki.

2.1.2 Mfumo wa Kupanga Bajeti

Mojawapo ya njia rahisi ya kupanga matumizi ya fedha kwa mwanafunzi ni kutumia mfumo wa **75-15-10.** Mfumo huu unasaidia kugawa fedha kwa uwiano unaozingatia mahitaji ya sasa, usalama wa baadae na matumizi binafsi. Ni mfumo rahisi unaoweza kutumiwa na mwanafunzi wa chuo anayepokea fedha kutoka HESLB, wazazi, ufadhili au shughuli za kujiongezea kipato.

Mfano: Mwanafunzi amepokea awamu ya kwanza ya mkopo wa HESLB wenye jumla ya Sh 600,000, fedha ambazo zinatarajiwa kumhudumia kwa kipindi cha miezi miwili. Hii ina maana kwamba, mwanafunzi anapaswa kupanga matumizi yake kwa wastani wa Sh 300,000 kwa mwezi. Kwa kutumia mfumo wa **75-15-10**, mgawanyo wa fedha unaweza kuwa kama ifuatavyo:

1. Akiba

Kwanza kabisa tenga asilimia kumi na tano (15%) sawa na Sh 45,000 kama akiba. Zingatia kwamba akiba ni fedha inayotengwa kwa ajili ya kukupa usalama wa kifedha na kukusaidia kujiandaa kwa malengo ya baadaye.

> **Kumbuka:** ***Akiba si fedha inayobaki baada ya matumizi; ni fedha inayotengwa kabla ya matumizi.***

2. Matumizi Muhimu

Baada ya kutenga akiba, hatua inayofuata ni kutenga fedha kwa ajili ya matumizi muhimu. Kwa kila Sh 300,000 unazopata kwa mwezi, asilimia sabini na tano (75%), sawa na Sh 225,000, inashauriwa kuelekezwa kwenye mahitaji muhimu. Hii ni sehemu ya bajeti inayogharimia mahitaji ya msingi ambayo ni muhimu kwa maisha na mafanikio yako ya masomo ukiwa chuoni. Mifano ya matumizi muhimu ni:

i. Chakula
ii. Malazi
iii. Nauli na usafiri
iv. Vitabu na vifaa vya masomo
v. Internet kwa ajili ya masomo

> **Kumbuka:** ***Mahitaji haya ndiyo msingi wa maisha yako ya chuo na mafanikio yako kitaaluma, hivyo yanapaswa kupewa kipaumbele cha kwanza kabla ya matumizi mengine yote.***

3. Matumizi ya Hiari

Asilimia kumi (10%) iliyobaki, sawa na Sh 30,000, inaweza kutumika kwa matumizi ya hiari. Hii ni sehemu ya fedha inayokuruhusu kufurahia maisha kwa kiwango kinachofaa bila kuathiri malengo yako ya kifedha. Inaweza kutumika kwa:

i. Burudani
ii. Mavazi ya gharama
iii. Zawadi
iv. Matumizi mengine binafsi

> ***Kumbuka: Matumizi ya hiari yasiwe sababu ya kuharibu bajeti yako au kukufanya ushindwe kutimiza mahitaji muhimu.***

Jedwali lifuatalo linaonyesha mfano mzuri wa namna ambayo mwanafunzi anaweza kupanga bajeti yake kwa kila mwezi.

Kitengo	Asilimia	Mwezi wa Kwanza (Sh 300,000)	Mwezi Wa Pili (Sh 300,000)	Mifano Ya Matumizi Kwa Mwezi
Matumizi Muhimu	75%	Sh 225,000	Sh 225,000	Chakula Sh 150,000 Nauli Sh 25,000 Malazi Sh 50,000
Akiba	15%	Sh 45,000	Sh 45,000	Akiba ya dharura na malengo ya baadae Sh 45,000
Matumizi ya hiari	10%	Sh 30,000	Sh 30,000	Mavazi ya gharama na matumizi ya hiari Sh 30,000
Jumla	**100%**	**Sh 300,000/=**	**Sh 300,000/=**	

> **Kumbuka:** ***Punguza matumizi yasiyo na ulazima kama kununua 'simu kali' au kubadilisha mavazi kila mwezi, hizi ni gharama zisizo na umuhimu.***

2.1.3 Athari za kutokuwa na bajeti.

Mwanafunzi asipokuwa na bajeti, athari zifuatazo zinaweza kutokea:

1. **Matumizi yasiyo na mpangilio:** Bila kuwa na bajeti, mwanafunzi anaweza kutumia fedha bila kuzingatia vipaumbele, hivyo fedha kuisha kabla ya kutimiza mahitaji muhimu au kabla ya kipindi kilichopangwa.

2. **Kuongezeka kwa uwezekano wa kuingia kwenye madeni:** Fedha zinapoisha kabla ya kutimiza mahitaji muhimu au kabla ya muda uliopangwa inaongeza uwezekano wa mwanafunzi kukopa ili kugharimia matumizi ya lazima.

3. **Kushindwa kufikia malengo ya kifedha:** Bila bajeti, inakuwa vigumu kujenga nidhamu ya kuweka akiba au kutenga fedha kwa ajili ya kujiendeleza kiuchumi.

4. **Msongo wa mawazo na kuathiri masomo:** Changamoto za kifedha zinazotokana na kukosa bajeti zinaweza kusababisha msongo wa mawazo, kupunguza umakini, na kuathiri maendeleo ya masomo.

Maswali

1. Ni jambo gani linaamua zaidi ustawi wa kifedha wa mwanafunzi?
    a. Kiasi kikubwa cha mkopo alichopata
    b. Kiasi cha fedha anachopokea kutoka kwa wazazi
    c. Namna anavyopanga na kutumia fedha zake
    d. Idadi ya marafiki alionao
2. Ni ipi kati ya hatua zifuatazo ni ya kwanza katika kuandaa bajeti?
    a.Kuorodhesha vyanzo vyote vya fedha unavyotarajia kupata
    b. Kuweka akiba
    c.Kununua mahitaji muhimu
    d. Kukopa fedha za ziada
3. Iwapo mwanafunzi amepokea Sh 600,000, ni kiasi gani kinashauriwa kutengwa kama akiba?
    a. Sh 60,000
    b. Sh 120,000
    c. Sh 90,000
    d. Sh 300,000
4. Ni ipi kati ya yafuatayo ni matumizi muhimu kwa mwanafunzi?
    a. Simu mpya ya gharama kubwa
    b. Party ya kila wiki
    c. Chakula na malazi
    d. Mavazi ya kifahari
5. Fedha ya dharura hutengwa kwa ajili ya:
    a. Burudani
    b. Kununua nguo mpya
    c. Kukabiliana na changamoto zisizotarajiwa
    d. Kununua simu mpya
6. Ni ipi kati ya yafuatayo ni mfano wa matumizi ya hiari?
    a. Malazi
    b. Chakula
    c. Internet kwa masomo
    d. Burudani na zawadi

2.2 Akiba

Maisha ya chuo huambatana na changamoto mbalimbali za kifedha. Wanafunzi wengi hupokea fedha kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, wazazi au walezi. Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa mipango mizuri ya matumizi, baadhi ya wanafunzi hujikuta wakikosa fedha kabla ya mwisho wa mwezi au muhula.



Akiba ni sehemu ya fedha iliyotengwa na kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadae. Kuna aina mbili (2) za akiba ambazo ni Akiba ya dharura na Akiba ya maendeleo.

2.2.1 Akiba ya Dharura

Hii ni aina ya akiba inayowekwa kwa ajili ya matumizi yasiyotarajiwa. Mwanafunzi anaweza kutenga kiasi fulani cha pesa kila mwezi kwa ajili ya mahitaji ya dharura. Mifano halisi ya matumizi ya fedha ya dharura ni kusaidia iwapo simu au Komputa Mpakato itaharibika na kuhitaji matengenezo ya haraka, nauli ya dharura kwa safari ya ghafla kwenda nyumbani kutokana na matatizo ya kifamilia, kununua mahitaji muhimu endapo fedha za matumizi zitachelewa kupatikana.

2.2.2 Akiba ya Maendeleo

Hii ni akiba inayotengwa kwa ajili ya kufanikisha malengo ya baadae. Mwanafunzi anaweza kutenga akiba kwa ajili ya kuanzisha biashara ndogo baada ya kuhitimu masomo yake. Mifano halisi ya matumizi ya fedha ya maendeleo ni kununua kompyuta mpakato (Laptop) kwa matumizi ya masomo, kuanzisha biashara ndogo baada ya kuhitimu, kulipia mafunzo ya ziada kama kozi za kompyuta, lugha za kigeni au ujasiriamali, kujiendeleza na masomo ya elimu ya juu zaidi, kununua vifaa vya kitaaluma kama kamera, vifaa vya maabara au vitabu.

2.2.3 Mambo Ya Kuzingatia Ili Kuweka Akiba

1. **Tambua kipato chako:** Mwanafunzi anatakiwa kutambua na kuainisha vyanzo vyake vyote vya fedha kama vile mkopo. Mfano Sh 300,000 kwa mwezi mkopo kutoka HESLB.

2. **Tambua matumizi yako:** Mwanafunzi anapaswa kutambua na kuainisha jinsi atakavyotumia fedha zake. Jedwali lifuatalo linaonyesha mfano wa mchanganuo wa matumizi kwa mwezi.

Kitengo	Asilimia	Mwezi Wa Kwanza (Sh 300,000)	Mwezi Wa Pili (Sh 300,000)	Mifano Ya Matumizi Kwa Mwezi
Matumizi Muhimu	75%	Sh 225,000	Sh 225,000	Chakula Sh 150,000 Nauli Sh 25,000 Malazi 50,000
Akiba	15%	Sh 45,000	Sh 45,000	Akiba ya dharura na malengo ya baadae Sh 45,000
Matumizi ya hiari	10%	Sh 30,000	Sh 30,000	Mavazi ya gharama na matumizi ya hiari Sh 30,000
Jumla	**100%**	**Sh 300,000/=**	**Sh 300,000/=**	

3. **Weka kiasi maalum cha akiba:** Inashauriwa kutenga angalau asilimia 15% ya fedha zako kwa ajili ya akiba.

4. **Chagua sehemu salama ya kuhifadhi akiba:** Weka akiba katika mifuko ya uwekezaji ya pamoja, akaunti ya akiba (benki), SACCOS, VIKOBA au mifumo mingine salama ya kifedha.

2.2.4 Umuhimu wa Akiba

Akiba ni muhimu sana kwa mwanafunzi kwa sababu humsaidia kutimiza malengo yake ya kielimu na maisha kwa ujumla. Jambo la kwanza, akiba humsaidia mwanafunzi kupata fedha za kutekeleza malengo aliyojiwekea kama kununua Komputa Mpakato au vitabu. Pili, mwanafunzi mwenye akiba anaweza kugharimia baadhi ya mahitaji yake bila kutegemea wazazi, walezi au marafiki kila wakati. Tatu, kuweka akiba humfundisha mwanafunzi kuwa

na nidhamu ya matumizi ya fedha kwa kupanga matumizi yake vizuri na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima. Nne, akiba humwezesha mwanafunzi kujenga msingi wa kifedha kwa ajili ya mipango ya baadaye kama biashara, kazi au kujiendeleza kimasomo. Mwisho, akiba humsaidia mwanafunzi kupunguza msongo wa mawazo. Mwanafunzi mwenye akiba huwa na utulivu zaidi kwa kuwa ana uhakika wa fedha za kumsaidia kukabiliana na changamoto za kifedha zinazoweza kujitokeza wakati wowote.

2.2.5 Changamoto za Kutokuweka Akiba

Mwanafunzi asiyeweka akiba hupata changamoto katika kufanikisha masomo yake na maisha kwa ujumla. Jambo la kwanza, mwanafunzi anaweza kuingia kwenye madeni kirahisi anapokosa akiba, kwani analazimika kukopa fedha ili kukidhi mahitaji yake ya dharura yanapojitokeza. Madeni yanaweza kuongezeka na kumletea mzigo mkubwa wa kurejesha. Pili, mwanafunzi hupata msongo wa mawazo pindi anapokosa akiba wakati wa dharura, hali hii inaweza kusababisha wasiwasi na kupunguza umakini katika masomo yake.Tatu, mwanafunzi anaweza kukosa fursa muhimu katika maisha kama kuhudhuria mafunzo ya ziada au safari za masomo. Mwisho, mwanafunzi anaweza kulazimika kuingia katika tabia zisizofaa zinazoweza kusababisha kutafuta njia zisizo sahihi za kupata fedha pale mahitaji ya dharura yanapojitokeza.

2.2.6 Hitimisho

Akiba ni nyenzo muhimu katika maisha ya mwanafunzi kwani humsaidia kuwa na usalama wa kifedha, kukabiliana na dharura, na kufanikisha malengo yake ya kielimu na ya baadaye. Kuweka akiba si suala la kuwa na fedha nyingi, bali ni kuwa na nidhamu ya kutenga sehemu ya fedha zinazopatikana kwa matumizi ya baadaye. Mwanafunzi anayejenga utamaduni wa kuweka akiba mapema hujiandaa vyema kwa maisha baada ya kuhitimu na hupunguza hatari zitokanazo na ukosefu wa fedha. Hivyo, mwanafunzi anashauriwa kupanga matumizi yake vizuri na kutenga sehemu ya fedha kwa ajili ya akiba ili kujenga msingi imara wa maendeleo yake binafsi na kitaaluma.

***Wewe Ndo Future, Timiza Wajibu wako*!**

Maswali

1. Akiba ni nini?

    a. Fedha zote zinazopatikana kwa mwezi

    b. Sehemu ya fedha inayotengwa na kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye

    c. Fedha za mkopo pekee

    d. Fedha zinazotumika kununua chakula

2. Ni aina gani mbili za akiba zilizotajwa katika mada hii?

    a. Akiba ya benki na akiba ya nyumbani

    b. Akiba ya muda mfupi na muda mrefu

    c. Akiba ya dharura na akiba ya malengo

    d. Akiba ya biashara na akiba ya familia

3. Akiba ya dharura hutumika kwa ajili ya nini?

    a. Kuanzisha biashara baada ya kuhitimu

    b. Kununua nyumba

    c. Mahitaji yasiyotarajiwa au ya dharura

    d. Kulipia ada za shule za watoto

4. Mfano wa matumizi ya akiba ya dharura ni upi?

    a.Kununua gari jipya

    b. Kulipia kozi ya uzamili

    c.Kununua ardhi

    d. Kutengeneza simu au Komputa Mpakato iliyoharibika ghafla

5. Akiba ya malengo hutengwa kwa kusudi gani**?**

    a.Matumizi ya kila siku

    b. Kukidhi mahitaji ya dharura pekee

    c.Kufanikisha mipango ya baadaye

    d. Kulipa kodi ya nyumba

6. Hatua ya kwanza ya kuweka akiba ni ipi?

    a. Kufungua akaunti ya benki

    b. Kutambua kipato chako

    c. Kununua vitabu vya masomo

d. Kukopa fedha

7. Ni ipi kati ya zifuatazo ni sehemu salama ya kuhifadhi akiba?

a. Kwenye kabati

b. Kwa rafiki wa karibu

c. Kwenye pochi

d. Akaunti ya benki au SACCOS

8. Kati ya yafuatayo, lipi ni umuhimu wa kuweka akiba kwa mwanafunzi?

a. Kuongeza matumizi yasiyo ya lazima

b. Kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha

c. Kuongeza utegemezi kwa marafiki

d. Kuepuka masomo

9. Kati ya yafuatayo, upi ni mfano wa akiba ya maendeleo?

a. Kuweka akiba kwa ajili ya kununua Komputa Mpakato ikipata changamoto

b. Kuweka akiba kwa jili ya kugharimia maradhi

c. Kuweka akiba kwa ajili ya kugharimia upotevu wa simu ukipotea

d. Kuweka akiba kwa ajili ya kugharimia masomo ya elimu ya juu

10. Moja ya changamoto za kutokuweka akiba ni ipi?

a. Kuwa na utulivu wa kifedha

b. Kuongeza fursa za maendeleo

c. Kuingia kwenye madeni kutokana na mahitaji ya dharura

d. Kuimarisha mipango ya baadaye

2.3 Uwekezaji

Uwekezaji ni kitendo cha kuwekeza kwenye rasilimali fedha au biashara kwa matarajio ya kupata faida baadaye. Tofauti na akiba ya kawaida, uwekezaji unalenga kukuza thamani ya fedha kwa muda maalumu, ingawa huwa unaambatana na kiwango fulani cha hatari.



Kwa ujumla, fedha za matumizi ya karibu zinafaa zaidi kubaki kwenye akiba, wakati fedha za malengo ya muda mrefu zinashauriwa kuelekezwa kwenye uwekezaji kulingana na uwezo wa mtu kuvumilia hatari.

2.3.1 Dhana Muhimu Kuhusu Uwekezaji

2.3.1.1 Uhusiano kati ya faida na hatari

Uwekezaji wenye uwezekano wa kupata faida kubwa mara nyingi huambatana na hatari kubwa. Hii ndiyo maana mwekezaji anatakiwa kujua kiwango chake cha kuvumilia hasara kabla ya kuamua kuwekeza.

Kwa uwekezaji unaozingatia sharia (usiohusisha riba), mwekezaji anatakiwa kushiriki katika faida na hasara.

2.3.1.2 Kutenga rasilimali / fedha (Asset allocation)

Kutenga rasilimali ni kitendo cha kugawa fedha zako kwenye makundi tofauti ya uwekezaji kama vile mifuko ya uwekezaji wa pamoja, hisa, hatifungani, biashara, fedha taslimu n.k. Mgawanyo huu hutegemea malengo yako, muda wa uwekezaji, na uwezo wako wa kuvumilia hatari.

2.3.1.3 Kutawanya hatari (Diversification)

Hiki ni kitendo cha kuwekeza kwenye vyanzo tofauti vya uwekezaji ili kupunguza hatari ya kutegemea aina / eneo moja pekee. Kwa lugha rahisi: *usiweke mayai yote kwenye kikapu kimoja.*

2.3.1.4 Riba Limbikizi (Compound interest)

Hii ni faida unayopata juu ya faida ya awali pamoja na mtaji wako. Mfano: Ukiwekeza shilingi 1,000 na ukapata riba ya asilimia 5 kwa mwaka, utapata faida ya shilingi 50 mwisho wa mwaka (1,000 × 5% = 50). Hivyo, utakuwa na jumla ya shilingi 1,050 baada ya mwaka mmoja, na jumla ya 1,102.5 baada ya mwaka wa pili kwa sababu mwaka wa pili faida inahesabiwa juu ya 105, si 100 pekee. Riba limbikizi ni chachu ya uwekezaji inayoonesha nguvu kubwa ya kuanza mapema.

2.3.2 Baadhi ya Aina za Uwekezaji

2.3.2.1 Hisa

Unaponunua hisa, unakuwa sehemu ya umiliki wa kampuni. Hisa zinaweza kukuza mtaji kwa kiwango kikubwa zaidi kwa muda mrefu, lakini bei zake hubadilika mara kwa mara.

Kwa mwekezaji anayezingatia misingi na kanuni za Sharia (misingi na kanuni za Kiislamu), anaweza kuwekeza katika makampuni yanayofanya shughuli zinazozingatia misingi na kanuni hizo (Halal) na kuepuka yale yanayojihusisha na riba na shughuli zilizokatazwa.

2.3.2.2 Hati Fungani (Bond)

Hati fungani nyaraka ya uwekezaji inayotolewa na serikali au kampuni ili kukopa fedha kutoka wawekezaji kwa makubaliano ya kulipa riba na kurejesha mtaji baada ya muda uliokubaliwa. Mara nyingi bondi huonekana kuwa na utulivu zaidi, ingawa nazo si salama kwa 100%.

Aidha, kuna hati fungani zinazozingatia misingi na kanuni za Sharia (misingi na kanuni za Kiislamu), zinazojulikana kama Sukuk. Tofauti na hati fungani za kawaida, Sukuk hutegemea umiliki wa rasilimali halisi na uwekezaji katika shughuli za kiuchumi zinazoruhusiwa kwa mujibu wa misingi na kanuni hizo.

2.3.2.3 Dhamana zinazouzika sokoni (Cash Equivalents)

Hizi ni dhamana zinazoweza kubadilishwa kua fedha taslimu kwa urahisi na haraka.Hatari yake ni ndogo ya kupoteza thamani na pia muda mfupi wa kukomaa, mara nyingi chini ya miezi mitatu.

2.3.2.4 Mifuko ya uwekezaji wa pamoja (Mutual Funds)

Hii ni mifuko ya uwekezaji inayokusanya fedha kutoka kwa watu wengi na kuziweka pamoja katika mali mbalimbali kama hisa, hati fungani na vitega uchumi vingine. Mara nyingi husaidia kupunguza hatari kwa kutoa fursa ya kuwekeza sehemu mbalimbali.

2.3.3 Hatua Salama za Kuanza Uwekezaji

Tahadhari ya kwanza kabla ya hatua zote: Fedha za mkopo wa HESLB zimetolewa kwa madhumuni maalumu kama ada, malazi na mahitaji ya masomo. Hatua hizi za uwekezaji zinahusu akiba unayojiwekea (rejea mada ya bajeti), au kipato cha kazi ndogondogo/biashara zako). Zifuatazo ni hatua za uwekezaji:

2.3.3.1 Tathmini hali yako ya kifedha: Andika kipato chako chote (mkopo, msaada wa familia, kipato cha ziada), matumizi yako ya lazima, na madeni uliyonayo. Huwezi kuwekeza kwa usalama kama hujui fedha zako zinakwenda wapi. Bajeti ndiyo ramani ya kwanza.

2.3.3.2 Tenga kiasi cha fedha kwa ajili ya dharura: Kabla ya kuwekeza, tenga akiba ya dharura kwenye akaunti rahisi kufikiwa. Mfuko huu unakuepusha kuuza uwekezaji wako kwa hasara au kukopa ili kukabiliana na dharura inapotokea.

2.3.3.3 Weka malengo na muda wake: Jiulize, nawekeza kwa ajili ya nini, na nitahitaji fedha hizi lini? Malengo ya muda mfupi (chini ya mwaka mmoja) yanafaa kubaki kwenye akiba au dhamana za muda mfupi; malengo ya muda mrefu (miaka 3+) ndiyo yanafaa kuelekezwa kwenye uwekezaji wenye ukuaji mkubwa zaidi.

2.3.3.4 Tambua uwezo wako wa kuvumilia hatari: Kama kushuka kwa thamani ya uwekezaji wako kunaweza kukufanya ushindwe kuhimili au kuathiri masomo yako, chagua aina ya uwekezaji wenye hatari ndogo na tulivu zaidi kama vile mifuko ya uwekezaji wa pamoja, hatifungani, n.k. Kumbuka kanuni ya msingi uliyojifunza: faida kubwa = hatari kubwa.

2.3.3.5 Jielimishe na uchague vyombo halali vilivyosajiliwa tu: Hapa ndipo somo la upatu linapokutana na somo la uwekezaji. Kabla ya kuweka

shilingi yoyote, hakikisha 'scheme' ya uwekezaji imesajiliwa na kusimamiwa na mamlaka husika kama Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa masoko ya mitaji, na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa taasisi za fedha.

2.3.3.6 Anza kidogo, kwa ratiba maalum: Usisubiri kuwa na fedha nyingi ili kuanza kuwekeza; Wekeza kiasi kilekile kidogo mara kwa mara. Kwa nguvu ya riba limbikizi uliyojifunza awali, kuanza mapema na kidogo kunashinda kuanza baadaye na kingi.

2.3.3.7 Tawanya uwekezaji wako (diversification): Usiweke fedha zote kwenye uwekezaji mmoja au wa aina moja. Mifuko ya uwekezaji wa pamoja inafaa hasa kwa wanaoanza kwa sababu yenyewe tayari imetawanya fedha kwenye hisa, hatifungani na vitega uchumi mbalimbali.

2.3.3.8 Fuatilia na urekebishe (rebalancing). Angalau mara moja au mbili kwa mwaka, pitia mgawanyo wako. Baadhi ya mali hukua haraka kuliko nyingine na kubadilisha uwiano uliopanga; rudisha mgawanyo kwenye lengo lako ili hatari isiongezeke bila wewe kutambua.

2.3.3.9 Kuwa makini na ulaghai daima: Kabla ya kila uamuzi wa kuwekeza, jiulize maswali ya kichujio uliyojifunza kwenye sehemu ya upatu: Je, kuna waraka wa matarajio (prospectus) ulioidhinishwa na CMSA? Je, faida inayoahidiwa inalingana na uhalisia wa soko? Je, malipo yangu yanategemea kuwaingiza watu wengine? "Fursa" yoyote inayoshindwa kichujio hiki si uwekezaji ni upatu uliovaa suti.

2.3.4 Hitimisho

Uwekezaji si mchezo wa kubahatisha, ni mpango wa kukuza fedha kwa nidhamu, maarifa, na uvumilivu. Mwekezaji mzuri huanza kwa kuelewa malengo yake, hutambua kiwango chake cha hatari, hugawa uwekezaji wake kwa busara, na hufikiria muda mrefu badala ya kukimbilia matokeo ya haraka.

***Wewe Ndo Future, Timiza wajibu wako*!**

Maswali

1. Uwekezaji ni nini?

   a. Kutunza fedha zote nyumbani ili zisitumike.

   b. Kitendo cha kuwekeza fedha au rasilimali kwa matarajio ya kupata faida baadaye.

   c. Kukopa fedha kwa ajili ya matumizi ya kila siku.

   d. Kutumia fedha zote mara tu unapozipata.

2. Kanuni ipi inaeleza uhusiano kati ya faida na hatari katika uwekezaji?

   a. Faida kubwa huwa na hatari ndogo kila wakati.

   b. Hatari kubwa husababisha hasara kila wakati.

   c. Uwekezaji wenye uwezekano wa faida kubwa mara nyingi huambatana na hatari kubwa.

   d. Hatari na faida havina uhusiano wowote.

3. Riba limbikizi (Compound Interest) ni ipi?

   a. Riba inayolipwa mara moja tu mwishoni mwa uwekezaji.

   b. Faida inayohesabiwa kwa kutumia mtaji wa awali pekee.

   c. Faida inayopatikana juu ya mtaji pamoja na faida iliyokwisha kupatikana.

   d. Ada inayolipwa kwa taasisi ya fedha.

4. Ni ipi kati ya zifuatazo ni hatua muhimu kabla ya kuanza kuwekeza?

   a. Kuwekeza fedha zote za mkopo wa HESLB.

   b. Kutathmini hali ya kifedha, kuweka bajeti, na kutenga akiba ya dharura.

   c. Kuwekeza kwenye fursa yoyote inayoahidi faida kubwa.

   d. Kukopa fedha zaidi ili kuongeza mtaji wa uwekezaji.

5. Kwa mujibu wa somo, mwanafunzi anatakiwa kuhakikisha nini kabla ya kuwekeza?

   a. Awekeze kwenye taasisi yoyote inayotoa faida kubwa zaidi.

   b. Ahakikishe uwekezaji umesajiliwa na unasimamiwa na mamlaka husika kama CMSA au Benki Kuu ya Tanzania.

   c. Awekeze kwa siri bila kuwashirikisha wengine.

   d. Atumie fedha zote za matumizi ya kila siku kwenye uwekezaji.

2.4 Kukopa kwa Hekima

Katika maisha ya chuo unaweza kukutana na nyakati ambazo unahitaji fedha za ziada. Siku hizi kuna fursa nyingi za mikopo kupitia benki, taasisi za kifedha na majukwaa ya kidijitali. Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kwamba kupata mkopo ni rahisi, lakini kurejesha ndiyo changamoto kubwa kwa watu wengi.

2.4.1 Mambo Muhimu ya Kuzingatia Kabla ya Kukopa

Ingawa mkopo unaweza kusaidia kutatua changamoto za kifedha au kukuwezesha kufikia malengo fulani, ni muhimu kufahamu kwamba kila mkopo ni deni linalopaswa kurejeshwa. Hivyo, kabla ya kufanya uamuzi wa kukopa, chukua muda kutafakari na kujiuliza maswali yafuatayo:

1. **Je, nahitaji kweli mkopo huu?**

Kopa kwa sababu ya uhitaji halisi, si kwa sababu ya tamaa au ushawishi wa marafiki. Jiulize kama unaweza kuendelea bila mkopo huo au kama ni jambo la lazima.

2. **Je, nina uwezo wa kuurejesha?**

Mkopo wowote unaochukua leo ni wajibu wa kuurejesha kesho. Hakikisha una mpango wa kulipa bila kuathiri mahitaji yako muhimu kama chakula, malazi au masomo.

3. **Je, nimeelewa riba na gharama zote za mkopo?**

Soma masharti yote kwa makini. Fahamu kiwango cha riba, muda wa kulipa, ada mbalimbali na adhabu za kuchelewa kulipa.

4. **Je, mkopo huu utanisaidia au utaniongezea matatizo?**

Mkopo mzuri ni ule unaosaidia kutatua tatizo muhimu au kufanikisha lengo lenye manufaa. Mkopo usio na sababu za msingi unaweza kuwa chanzo cha matatizo ya ***kifedha baadaye.***

> **Kumbuka:** ***Kama jibu la mojawapo ya maswali hayo ni HAPANA, fikiria tena kabla ya kukopa.***

2.4.2 Jinsi ya Kutambua Mkopo Salama

Siyo kila mkopo unaotolewa ni salama. Baadhi ya mikopo inaweza kuwa na masharti magumu au gharama kubwa zinazoweza kukuingiza kwenye changamoto za kifedha.

Mambo ya kuzingatia kabla ya kukopa ni kama yafuatayo:

1. Hakikisha unakopa kwa mkopeshaji mwenye leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania;
2. Zingatia lengo la mkopo na epuka kuchukua mkopo kwa matumizi yasiyo ya lazima;
3. Soma na elewa mkataba au masharti ya mkopo kabla ya kusaini ikiwemo riba na gharama nyinginezo;
4. Linganisha taasisi mbalimbali za mikopo; na
5. Jipime uwezo wa kulipa mkopo wote kwa wakati.

> **Tahadhari:** ***Usikubali kukopa kwa sababu tu fedha zinapatikana kirahisi. Kopa pale tu ambapo kuna sababu ya msingi na uwezo wa kulipa.***

2.4.3 Kituo cha Taarifa za Mikopo (Credit Reference Bureau)

Credit Reference Bureau (CRB) ni mfumo wa ukusanyaji na uhifadhi wa taarifa za mikopo ya wakopaji. Mfumo huu huonyesha historia yako ya kukopa na kurejesha madeni. Kwa lugha rahisi, CRB ni ripoti ya tabia yako ya kukopa na kulipa madeni. Watu wengi hufikiri kwamba historia ya mikopo ni jambo la watu wenye biashara kubwa au wafanyakazi pekee. Ukweli ni kwamba kila mkopo unaochukua na jinsi unavyoulipa hujenga sifa yako ya kifedha.

Jedwali hili hapa chini linaonyesha matokeo ya kulipa au kutokulipa mkopo wako kwa wakati.

Ukilipa kwa Wakati	Ukichelewa Kulipa
Sifa yako ya kifedha huongezeka.	Sifa yako ya kifedha hupungua.
Uwezekano wa kupata mikopo mingine huongezeka.	Unaweza kukataliwa unapohitaji mkopo mwingine.
Taasisi za kifedha hujenga imani kwako.	Fursa nyingi za kifedha zinaweza kukupita.

Matokeo ya mtu anayechelewesha kulipa mkopo au kushindwa kulipa kwa wakati kutakusabisha ushindwe kupata mikopo mingine. Kwa mfano:-

i. Mkopo wa biashara
ii. Mkopo wa nyumba
iii. Mkopo wa gari
iv. Mikopo mingine ya maendeleo
v. Huduma mbalimbali za kifedha siku zijazo

> **Kumbuka:** ***Tabia yako ya kifedha ya leo inaweza kuamua fursa zako za kifedha za kesho.***

2.4.4 Ujumbe Muhimu Kuhusu Mkopo wa HESLB

Mkopo wa HESLB si zawadi wala msaada wa bure. Ni uwezeshaji unaofanywa na Serikali ya Tanzania ili kuwasaidia vijana wa Kitanzania kupata elimu ya juu na kutimiza ndoto zao.

Fedha hizi hutolewa kwa makubaliano kwamba mara baada ya kupata kipato au miaka miwili baada ya kuhitimu, mnufaika atazirejesha ili wanafunzi wengine wenye uhitaji wapate fursa hiyo. Hivyo kwa kurejesha mkopo wako kwa wakati:

i. Unawasaidia Watanzania wengine kupata elimu.
ii. Unachangia maendeleo ya sekta ya elimu nchini.
iii. Unatimiza wajibu wako kwa Taifa.
iv. Unakuwa sehemu ya kujenga kizazi kijacho cha wasomi na wataalamu.

> **Kumbuka:** ***Mkopo wa HESLB ni daraja la mafanikio yako; tumia vizuri leo na urejeshe kwa uwajibikaji kesho.***

2.4.5 Mambo ya Kuzingatia

i. Andaa bajeti kabla hujapokea fedha ili kupanga mapato na matumizi yako.
ii. Weka akiba kwanza kabla ya kufanya matumizi mengine yoyote.
iii. Rejesha mkopo wa HESLB kwa wakati ili kuwapa wanafunzi wengine wahitaji fursa ya kusoma.

Wewe Ndo Future, Timiza Wajibu wako!

Maswali

1. Kabla ya kukopa, mwanafunzi anapaswa kujiuliza swali gani muhimu?
    a. Je, marafiki zangu wanakopa?
    b. Je, mkopo huu utanifanya nionekane tajiri?
    c. Je, nina uwezo wa kuurejesha?
    d. Je, nitapata simu mpya?

2. Ni ipi kati ya sifa zifuatazo inaonyesha mkopo salama?
    a. Riba kubwa sana
    b. Masharti yasiyoeleweka
    c. Taasisi isiyojulikana
    d. Riba na gharama za mikopo imeelezwa wazi na taasisi imesajiliwa

3. Kwa nini ni muhimu kurejesha mkopo wa HESLB kwa wakati?
    a. Ili kupata mkopo mwingine mara moja
    b. Ili kuepuka kusoma tena
    c. Ili kuwasaidia Watanzania wengine kupata fursa za mikopo
    d. Ili kuongeza kiasi cha mkopo wako

2.5 Kujilinda Dhidi ya Utapeli wa Kifedha na Upatu Haramu



Utapeli wa kifedha ni kitendo cha mtu au kikundi cha watu kutumia udanganyifu ili kupata fedha, taarifa za kifedha au mali za wengine kinyume cha sheria. Mara nyingi matapeli hutumia uongo, ahadi zisizo za kweli, utambulisho bandia au teknolojia kuwashawishi watu kutoa fedha au kufichua taarifa zao za siri. Tofauti na wizi wa kawaida, utapeli wa kifedha humfanya mwathirika kutoa fedha au taarifa kwa hiari kwa sababu anaamini kuwa anayewasiliana naye ni mtu au taasisi halali.

Utapeli unaweza kufanyika kupitia simu, ujumbe mfupi (SMS), Mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, Facebook na Instagram, barua pepe au tovuti zinazofanana na zile za taasisi halali. Wakati mwingine matapeli hujifanya wafanyakazi wa benki, kampuni za simu, taasisi za Serikali au hata marafiki na ndugu.

Kadiri matumizi ya huduma za kifedha kidijitali yanavyoongezeka nchini Duniani, ndivyo mbinu za utapeli nazo zinavyoendelea kubadilika. Hivyo, kila mtumiaji wa huduma za kifedha anatakiwa kuwa makini wakati wote.

2.5.1 Sifa Kuu za Utapeli wa Kifedha

Ingawa mbinu za utapeli hubadilika mara kwa mara, matapeli wengi hutumia mbinu zinazofanana. Kutambua sifa hizi kunaweza kukusaidia kuepuka hasara kubwa.

i. **Ahadi za kupata faida kubwa kwa muda mfupi bila hatari yoyote:** Katika uwekezaji halali hakuna faida inayohakikishwa bila kuwepo kwa kiwango fulani cha hatari.

ii. **Kuharakisha watu kufanya maamuzi:** Matapeli wanaweza kusema kuwa nafasi ni ya muda mfupi au kwamba lazima utume fedha mara moja ili usipoteze fursa.

iii. **Kuomba taarifa za siri kama namba ya siri (PIN), nenosiri la benki, namba ya uthibitisho wa miamala (OTP), au taarifa za kadi za benki**. Taasisi halali za kifedha hazitoi maombi ya aina hii kupitia simu, WhatsApp, SMS au mitandao ya kijamii.

iv. **Kutuma fedha kwanza ili upokee mkopo, zawadi, ajira au huduma fulani.** Mara nyingi baada ya kutuma fedha hizo, mawasiliano hukatika na fedha hupotea.

> **Kumbuka:** ***Ikiwa jambo linaonekana kuwa zuri kupita kiasi au linaahidi faida kubwa bila hatari, kuna uwezekano mkubwa kuwa ni utapeli.***

2.5.2 Aina za Utapeli wa Kifedha Kidijitali

Maendeleo ya teknolojia yameongeza aina mbalimbali za utapeli wa kifedha unaofanyika kupitia vifaa vya kidijitali kama ifuatavyo:

i. **Phishing (Barua Pepe au Tovuti Bandia)**

ii. Hii ni mbinu ya kutuma barua pepe au kutengeneza tovuti bandia zinazofanana na zile za taasisi halali ili kuiba taarifa za kifedha.Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kupokea barua pepe inayodai kutoka HESLB ikimtaka athibitishe taarifa za akaunti yake kwa kubofya kiungo (link). Kiungo hicho humpeleka kwenye tovuti bandia inayokusanya taarifa zake za benki.

iii. **Smishing (Ujumbe Mfupi wa Udanganyifu)**

iv. Hii ni aina ya phishing inayotumia ujumbe mfupi wa simu (SMS).Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kupokea ujumbe unaosema:

v. *“Hongera! Umepata ufadhili maalumu. Bonyeza hapa kudai fedha zako.”*

vi. Baada ya kubonyeza kiungo hicho, taarifa zake binafsi au fedha zake huibiwa.

vii. **Vishing (Utapeli Kupitia Simu)**

viii. Katika mbinu hii, matapeli hupiga simu wakijifanya ni wafanyakazi wa benki au kampuni ya simu na kudai kuwa kuna tatizo kwenye akaunti yako.

ix. Baadaye watakuomba utoe PIN au namba ya uthibitisho wa muamala (OTP). Ukitoa taarifa hizo, wanaweza kufanya miamala kwenye akaunti yako bila idhini yako.

x. Social Engineering (Udanganyifu wa Kisaikolojia)

xi. Hii ni mbinu inayotumia hisia za binadamu badala ya kuvamia mifumo ya kompyuta.Matapeli wanaweza kutumia hofu, huruma, shinikizo au mamlaka ili kukushawishi utoe fedha au taarifa zako.Kwa mfano, mtu anaweza kujifanya ni kiongozi wa chuo na kukuambia ulipe ada ya usajili haraka ili usifutiwe usajili wa masomo.

xii. Fursa Bandia za Uwekezaji

xiii. Matapeli wengi hutangaza uwekezaji unaoahidi faida kubwa ndani ya muda mfupi kupitia mitandao ya kijamii.Ni muhimu kufahamu kuwa uwekezaji halali hauwezi kuahidi faida kubwa za uhakika bila hatari.

xiv. Wizi wa Utambulisho (Identity Theft)

xv. Wahalifu wanaweza kuiba taarifa zako binafsi kama Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), taarifa za akaunti ya benki, namba ya simu au nakala za vitambulisho na kuzitumia kufanya udanganyifu. Taarifa hizi zinaweza kutumika kuchukua mikopo, kusajili laini za simu au kufanya miamala ya kifedha bila idhini yako.

xvi. Utapeli wa Sauti unaotumia Akili Unde (AI Voice Fraud)

Teknolojia ya Akili Unde (Artificial Intelligence - AI) imewezesha matapeli kuiga sauti za watu kwa usahihi mkubwa. Kwa kutumia sekunde chache za sauti zilizorekodiwa kwenye mitandao ya kijamii, matapeli wanaweza kutengeneza sauti inayofanana kabisa na ya mzazi, ndugu au rafiki. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kupigiwa simu na mtu anayesikika kama mzazi wake akidai kuwa amepata dharura na anahitaji fedha haraka. Bila kuthibitisha ukweli wa taarifa hiyo, mwanafunzi anaweza kutuma fedha kwa matapeli.

Unapopokea ombi la fedha, hata kama sauti inaonekana ya mtu unayemfahamu, hakikisha unathibitisha taarifa hiyo kupitia njia nyingine ya mawasiliano kabla ya kutuma fedha.

2.5.3 Namna ya Kujilinda Dhidi ya Utapeli wa Kifedha

Zifuatazo ni njia bora ya kujikinga dhidi ya utapeli wa kifedha:

i. Usimpe mtu yeyote PIN, nenosiri au namba ya uthibitisho wa muamala (OTP) hata kama anayezihitaji anajitambulisha kuwa mfanyakazi wa benki au kampuni ya simu;

ii. Kabla ya kufanya uwekezaji au kutuma fedha, hakikisha taasisi au kampuni unayoshughulika nayo imesajiliwa na inasimamiwa na mamlaka husika;

iii. Epuka kubofya viungo usivyovijua vinavyotumwa kupitia SMS, WhatsApp au barua pepe. Hakikisha anwani ya tovuti ni sahihi kabla ya kuingiza taarifa zako binafsi.

iv. Epuka kufanya miamala ya kifedha kupitia mitandao ya Wi-Fi ya umma na hakikisha simu yako na programu za kifedha zinaendelea kuhuishwa (Updates) mara kwa mara ili kuongeza usalama.

2.5.4 Madhara ya Utapeli wa Kifedha

Utapeli wa kifedha unaweza kusababisha madhara yafuatayo kwa mwanafunzi:

i. Mwanafunzi anaweza kupoteza fedha za kujikimu na kushindwa kugharimia mahitaji muhimu kama chakula, malazi, usafiri na vifaa vya kujifunzia. Hali hii inaweza kuathiri maendeleo ya masomo na hata kusababisha mwanafunzi kuahirisha masomo.

ii. Mwanafunzi anaweza kuibiwa utambulisho wake na taarifa zake kutumika kufanya uhalifu mwingine wa kifedha.

iii. Utapeli unaweza kusababisha msongo wa mawazo, kupoteza imani katika huduma za kifedha na kuathiri historia ya matumizi ya huduma za kifedha.

> **Kumbuka:** ***kulipa fedha zinazodaiwa na wahalifu wa mtandao (ransomware) au matapeli hakuhakikishi kwamba fedha zako au taarifa zako zilizoibwa zitarudishwa.***

2.5.5 Kuripoti Utapeli wa Kifedha

i. Wasiliana mara moja na benki yako au mtoa huduma wa fedha kwa njia ya simu ili kusitisha akaunti au huduma husika ikiwa bado inawezekana. Hifadhi ushahidi wote kama ujumbe mfupi, barua pepe, namba za simu, risiti za miamala na picha za skrini.

ii. Toa taarifa kwenye Jeshi la Polisi na pia ripoti tukio kwa mamlaka husika kulingana na aina ya huduma iliyohusika. Ikiwa linahusu taasisi ya fedha iliyo chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania, taarifa inaweza kutolewa Benki Kuu ya Tanzania. Ikiwa linahusu uwekezaji au masoko ya mitaji, taarifa inaweza kutolewa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).

2.5.6 Hitimisho

Kadiri teknolojia inavyoendelea kukua, ndivyo mbinu za utapeli wa kifedha zinavyoendelea kubadilika. Hata hivyo, maarifa, umakini na kuchukua tahadhari ni silaha muhimu katika kujilinda dhidi ya matapeli. Mwanafunzi anayejifunza kutambua dalili za utapeli, kulinda taarifa zake binafsi, kuthibitisha uhalali wa taasisi za kifedha na kuripoti matukio ya udanganyifu kwa wakati, huongeza usalama wa fedha zake na mafanikio yake ya kielimu.

Elimu ya fedha haihusishi tu kujifunza namna ya kupata, kutumia, kuweka akiba na kuwekeza fedha, bali pia kujifunza namna ya kuzilinda dhidi ya utapeli.

Maswali

1. Ni ipi kati ya zifuatazo ni dalili ya utapeli wa kifedha?

    a. Taasisi ya fedha kukuomba kuthibitisha taarifa zako kupitia tawi rasmi.

    b. Kuahidi faida kubwa kwa muda mfupi bila hatari yoyote.

    c. Kupokea taarifa za akaunti kupitia programu rasmi ya benki.

    d. Kusoma masharti na vigezo vya huduma kabla ya kufanya muamala.

2. Mtu akikupigia simu na kujitambulisha kuwa mfanyakazi wa benki Kisha akakuomba umpe namba yako ya siri (PIN) na namba ya uthibitisho wa muamala (OTP) , unapaswa kufanya nini?

    a. Kumpa taarifa hizo ili akusaidie kutatua tatizo.

    b. Kumtumia taarifa hizo kupitia WhatsApp.

    c. Kukataa kutoa taarifa hizo na kuwasiliana na benki kupitia namba rasmi.

    d. Kumwomba akupigie baadaye.

3. Baada ya kugundua kuwa umetapeliwa kupitia mtandao, hatua ya kwanza unayopaswa kuchukua ni ipi?

    a. Kufuta ujumbe wote uliopokea.

    b. Kusitisha muamala au kuwasiliana mara moja na benki au mtoa huduma wa fedha.

    c. Kusubiri kuona kama fedha zitarudishwa.

    d. Kutuma fedha nyingine ili kurejeshewa zilizopotea.

2.6 Jihadhari na Upatu

Mada hii imeandaliwa ili kutoa uelewa na namna ya kutambua na kujiepusha na Upatu “pyramid schemes” na mipango mingine ya uwekezaji wa kitapeli inayolenga kupora akiba na fedha za mikopo ya wanafunzi. Pia utapata uelewa juu ya uwekezaji, aina zake za msingi, uhusiano wa hatari na faida, na hatua salama za kuanza kuwekeza.

Wanafunzi mara nyingi hulengwa na matapeli kwa sababu wanapokea fedha za mkopo kwa mkupuo. Matapeli hutoa ahadi ya faida maradufu ili kuwavutia wanafunzi kisha kuwaibia.

Takwimu za taifa zinaonyesha watanzania walipoteza takribani Shilingi bilioni 5.345 kwa utapeli wa kifedha mwaka 2024, na kupungua hadi Shilingi bilioni 4.778 mwaka 2025. Makosa mengi yalihusu miamala ya simu, njia ambayo wanafunzi hutumia kununua na kulipia huduma mbalimbali. Upatu ni kosa la jinai chini ya kanuni ya adhabu vifungu 171 (A-C), na adhabu yake yaweza kufikia kifungo cha miaka 20-30. Kupoteza fedha za mkopo kwenye upatu kunahatarisha masomo na usalama wako kisheria.

2.6.1 Maana ya Upatu

Upatu ni mpango wa kuchangisha fedha unaoendeshwa na mtu au kikundi cha watu kwa kuwadanganya wachangiaji kuwa watapata faida kubwa kwa muda mfupi. Kivutio kikubwa ni ahadi ya malipo makubwa bila mchangiaji kushiriki katika shughuli yoyote halisi ya uzalishaji.

Ili kushiriki, mchangiaji hutakiwa kutoa kiasi fulani cha fedha, kisha kushawishi watu wengine wajiunge kama yeye. Fedha za kila mshiriki mpya ndizo zinazotumika kuwalipa walioingia kabla yake.

2.6.2 Kiini cha Tatizo

Ili mtu mmoja alipwe, lazima wapatikane wachangiaji wengi wapya chini yake. Idadi inayohitajika huongezeka kwa kasi kubwa mno hadi inashindikana kupatikana ndipo mpango huanguka na wengi hupoteza fedha zao

Mfano wa Upatu.

Mchangiaji anatoa Sh. 50,000 na anaahidiwa kupewa Sh. 300,000 baada ya miezi mitatu. Ili kumlipa mchangiaji mmoja wa safu ya juu, wanahitajika wachangiaji 6 katika safu inayofuata; ili kuwalipa hao 6, wanahitajika 36 wengine; na kadhalika. Idadi inazidi kuongezeka mara sita kila safu.

Angalia jinsi namba zinavyokua kwa kasi:

Ngazi	Wachangiaji wapya	Jumla ya wachangiaji	Kiasi cha malipo (Sh)
1	1	1	50,000
2	6	7	300,000
3	36	43	1,800,000
4	216	259	10,800,000
5	1,296	1,555	64,800,000
6	7,776	9,331	388,800,000
Ngazi	**Wachangiaji wapya**	**Jumla ya wachangiaji**	**Kiasi cha malipo (Sh)**
7	46,656	55,987	2,332,800,000
10	10,077,696	12,093,235	503,884,800,000
13	2,176,782,336	2,612,138,803	108,839,116,800,000
16	470,184,984,576	564,221,981,491	23,509,249,228,800,000
17	2,821,109,907,456	3,385,331,888,947	141,055,495,372,800,000

Chanzo: Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

(Baadhi ya ngazi za kati zimerukwa ili kurahisisha kusoma jedwali.)

Hivyo, kufikia ngazi ya 17, mpango ungehitaji wachangiaji wapya zaidi ya trilioni 2.8, idadi inayozidi watu wote duniani kwa sasa! Hili haliwezekani. Kwa hiyo mpango wa aina hii ni lazima uanguke, na watu walio chini hupoteza fedha zao zote.

2.6.3 Tofauti Kati ya Upatu na Uwekezaji

Jedwali lifuatalo linaeleza tofauti ya upatu na uwekezaji:

Na.	Kipengele	Upatu	Uwekezaji
1.	Chanzo cha faida	Faida hutokana na michango ya wanachama wapya.	Faida hutokana na shughuli halisi za biashara, uzalishaji, huduma au miradi ya uwekezaji.
2.	Kiwango cha faida	Huahidi faida kubwa sana, za haraka na za uhakika bila maelezo ya msingi wake.	Faida hutegemea utendaji wa uwekezaji na hali ya soko; hakuna uhakika wa faida kubwa wakati wote.

Na.	Kipengele	Upatu	Uwekezaji
3.	Ufafanuzi wa biashara	Mara nyingi hauelezi wazi fedha zinavyozalisha mapato.	Huwa na maelezo ya wazi kuhusu biashara, mradi au mali inayowekezwa.
4.	Nyaraka za uwekezaji	Haina waraka wa matarajio (prospectus) au taarifa za kutosha.	Huwa na nyaraka rasmi zinazoeleza malengo, hatari na matarajio ya uwekezaji.
5.	Usajili na vibali	Inafanya biashara tofauti na iliyosajiliwa	Husajiliwa na kusimamiwa na mamlaka za Serikali zinazohusika mfano Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Benki Kuu ya Tanzania (BOT)
6.	Ushawishi wa wanachama wapya	Huwalazimisha au kuwahamasisha washiriki kusajili wanachama wapya ili kupata faida zaidi.	Faida haitegemei kusajili wanachama wapya pekee.
7.	Mikataba	Mara nyingi hakuna mkataba rasmi wa uwekezaji au wa kurejeshewa fedha.	Huwa na mikataba rasmi inayobainisha haki na wajibu wa pande zote.
8.	Hatari za uwekezaji	Huficha au kupuuza hatari za uwekezaji.	Hueleza wazi hatari zinazoweza kuathiri faida au mtaji uliowekezwa.
9.	Uendelevu	Huporomoka wanapopungua wanachama wapya.	Unaweza kuendelea kwa muda mrefu kwa sababu unategemea shughuli halisi za kiuchumi.
10.	Uwazi wa taarifa	Taarifa za kifedha mara nyingi hazipo au si za kuaminika.	Huwa na taarifa za kifedha na mifumo ya uwajibikaji inayoweza kuhakikiwa.

2.6.4 Aina na Upatu

Upatu huja kwa sura nyingi. Hapa ni mifano michache ya kawaida:

1. Mlolongo wa Barua (Chain Letters)

Unapokea barua (au siku hizi ujumbe wa simu/mtandao) inayokutaka kutuma fedha kwa watu waliotajwa, kuongeza jina lako kwenye orodha, na kusambaza ujumbe kwa wengine. Mara nyingi hudanganya kuwa “inatambulika kisheria”.

2. Mipango ya Ponzi / Klabu za Kupeana / "Networks"

Hizi huundwa kuwalipa washiriki wa kwanza kwa fedha za washiriki watakaojiunga baadaye. Kwa kuwa hakuna chanzo kingine cha fedha zaidi ya wachangiaji wapya, idadi ya wanachama wapya hupungua na klabu hufilisika.

2.6.5 Madhara ya Kushiriki Upatu

Kushiriki upatu si hatari kwa fedha zako tu, bali pia ni uamuzi unaoweza kukugharimu uhuru wako, masomo yako, na mustakabali wako mzima. Sheria za Tanzania zikiwemo Kanuni za Adhabu, Cap 16, kifungu 171A; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, 2003; na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, 1994; hazimhusu mwendeshaji wa upatu tu, zinawahusu pia anayeshiriki kwa kuchangia fedha na anayeshawishi watu kujiunga; wote hawa wanavunja sheria na ni makosa ya jinai. Madhara yake ni:

i. **Kifungo na rekodi ya jinai:** Mashtaka yanayohusiana na upatu na uhujumu uchumi yanaweza kusababisha kifungo cha hadi miaka 20 hadi 30 jela. Hata kama hutafungwa, kukamatwa na kufunguliwa kesi kunakuachia rekodi ya jinai inayoweza kukufungia milango ya ajira serikalini, kwenye taasisi za fedha, na hata fursa za masomo nje ya nchi.

ii. **Kupoteza fedha**: Kwa kuwa kushiriki upatu ni kosa la jinai, ni vigumu kwenda polisi au mahakamani kudai fedha zilizopotea. Hii ndiyo sababu waathirika wengi hukaa kimya, na ndiyo maana takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mabilioni yanayopotea kwa utapeli kila mwaka huku fedha zinazorejeshwa ni chini ya asilimia 5. Fedha ikishaingia kwenye upatu, ihesabu imepotea.

iii. **Kuhatarisha masomo na mkopo wako:** Fedha za mkopo wa HESLB ni fedha za umma ulizokabidhiwa kwa madhumuni maalum ya elimu. Ukizipoteza kwenye upatu, hutakuwa na fedha ya kukuwezesha kuendelea na masomo kama ilivyokusudiwa na mkopo huo utabaki kuwa deni lako la kurejesha hata kama fedha zenyewe ziliibiwa. Wanafunzi wengi waliopoteza fedha kwa njia hii wamelazimika kuacha au kuahirisha masomo.

iv. **Kuwa chombo cha kuwadhuru wengine:** Muundo wa upatu unakulazimisha kuwashawishi wengine kama vile ndugu, marafiki na wanafunzi wenzako wajiunge ili wewe ulipwe. Mpango unapoanguka, ikiwa umeshiriki kuwashawishi kujiunga na upatu, unaweza kupoteza uaminifu, mahusiano na heshima yako kwao na kwa jamii.


v. **Madhara kwa taifa:** Fedha zinazoingia kwenye upatu hutolewa kwenye shughuli rasmi za uzalishaji.

2.6.6 Taarifa na Kupata Msaada

Endapo unatilia shaka fursa yoyote ya uwekezaji au unashawishiwa kujiunga na mpango wenye sura ya upatu, wasiliana na mojawapo ya taasisi zifuatazo:

Taasisi	Mawasiliano	Tovuti
Jeshi la Polisi (Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai)	Simu: 0732 999154	www.policeforce.go.tz
Benki Kuu ya Tanzania (BoT)	Simu: (22) 2233000/20	www.bot.go.tz
Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)	Simu: (22) 2114959/61 Barua pepe: info@cmsa-tz.org	www.cmsa-tz.org

2.6.7 Hatua za Kujilinda na Upatu



2.6.8 Hitimisho

Kila shilingi ya mkopo wa mwanafunzi inayopotea kwenye upatu ni shilingi iliyokusudiwa kurejeshwa ili kumsomesha mwanafunzi mwingine. Pia, sheria haijaweka adhabu hizi ili kukutisha bila sababu, bali kihisabati upatu, lazima uwaibie walio wengi ili kuwalipa wachache. Hivyo, ukishiriki, unapoteza mara tatu: fedha zako, ulinzi wa kisheria, na uhalali wako mbele ya sheria.

Wewe Ndo Future, Timiza Wajibu wako!

Maswali

1. Kipato cha Upatu unategemea zaidi nini?
    a. Biashara ya uzalishaji
    b. Michango ya wanachama wapya
    c. Riba ya benki
    d. Uagizaji bidhaa
2. Ipi sifa kuu ya Upatu?
    a. Uwekezaji wenye hatari ndogo
    b. Faida hutokana na biashara halisi
    c. Ahadi ya faida kubwa bila maelezo ya msingi
    d. Uendeshaji na serikali
3. Upatu huwalenga zaidi watu gani?
    a. Wakulima wakubwa
    b. Wafanyabiashara wakubwa tu
    c. Wanafunzi na watu wenye uelewa mdogo wa masuala ya kifedha.
    d. Mabenki
4. Faida ya uwekezaji halali hutokana na nini**?**
    a. Michango ya wanachama wapya
    b. Biashara halisi na uzalishaji
    c. Ulaghai wa mtandao
    d. Bahati na kubahatisha
5. Ni **ipi kati ya zifuatazo ni hatua sahihi ya kujilinda na Upatu?**
    a. Kujiunga haraka ili kupata faida kubwa
    b. Kuchukua mkopo ili kuwekeza zaidi
    c. Kuchunguza uhalali wa uwekezaji kabla ya kujiunga
    d. Kuwashawishi marafiki wengi waingie

2.7 Kipato

Kipato ni fedha au rasilimali anayopata mtu, familia au taasisi kutokana na kazi, biashara, au uwekezaji. Ni nguvu inayosukuma maendeleo ya mtu binafsi na Taifa kwa ujumla.

2.7.1 Faida za kuwa na Kipato



i. **Kukidhi mahitaji ya msingi**: kipato hutumika kununua chakula, mavazi, makazi, huduma za afya na elimu kama vile vitabu na vitendea kazi kama Komputa Mpakato.

ii. **Kuboresha maisha**: husaidia mtu kupata maisha bora na kuongeza ustawi wa familia.

iii. **Kuweka akiba:** sehemu ya kipato inaweza kuwekwa akiba kwa matumizi ya baadaye ikiwa ni pamoja dharura.

iv. **Kuwezesha uwekezaji:** kipato kinaweza kutumika kuanzisha biashara au kuwekeza katika miradi mbalimbali ili kuongeza kipato.

v. **Kufanikisha malengo ya maisha:** huwezesha mtu kufikia malengo kama kununua nyumba, gari au kujiendeleza kielimu zaidi.

vi. **Kuchangia maendeleo ya jamii na Taifa:** kupitia kodi na matumizi mbalimbali, kipato huchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

2.7.2 Vyanzo Vya Kipato (Fedha) Kwa Mwanafunzi

i. Mkopo kutoka HESLB.

ii. Ufadhili wa elimu ya juu kutoka vyanzo mbalimbali kama taasisi, watu binafsi.

iii. Akiba mbalimbali.

iv. Faida itokanayo na uwekezaji mbalimbali.

v. Fedha za kujikimu kutoka kwa wazazi.

vi. Biashara mbalimbali.

vii. Sehemu za mafunzo ya kazi (internship).

viii. Kazi za muda mfupi (part time job).

ix. Vyanzo vingine mfano: kilimo na ufugaji.



2.7.3 Faida na Hasara za Vyanzo mbalimbali vya Kipato (Fedha)

Kipato kinaweza kuwa kipato tulivu (Passive income) au hai (Active income). Kipato tulivu ni kipato ambacho huendelea kuingia hata kama mtu hafanyi kazi moja kwa moja kila siku. Mara nyingi hutokanana uwekezaji au mali zinazozalisha mapato kwa muda mrefu. Mfano; kodi ya pango, faida za hisa (dividends), riba kutoka akiba au amana za benki, mapato kutokana na mauzo ya vitabu, kozi, au muziki yaliyofanyika kwa njia ya mtandao, faida kutoka biashara inayosimamiwa na wengine. Hii ni muhimu sana kwani huongeza uhuru wa kifedha, hupunguza utegemezi wa mshahara na huweza kuendelea hata ukiwa umestaafu, nyakati za dharura au ugonjwa/ajali.

Kipato hai ni kile unachopata kwa kubadilishana muda au nguvu zako na malipo. Ukiacha kufanya kazi, kipato nacho husimama. Mfano; mshahara wa mwajiriwa, malipo ya kazi za muda mfupi (part-time jobs), malipo ya ushauri (consultancy) na biashara ambayo mmiliki anahusika moja kwa moja kwenye uzalishaji.

S/N	Chanzo	Faida	Hasara
1.	Mkopo kutoka HESLB	- kuwezesha kupata elimu ya juu - kupunguza utegemezi wa fedha wa moja kwa moja kwa familia - kugharimia mahitaji muhimu	- Huongeza mzigo wa deni baada ya masomo - Hutozwa gharama ya mkopo kama gharama ya uendeshaji - Inaweza kuathiri uwezo wa kukopesheka kwa mnufaika, ikiwa hatazingatia masharti ya mkataba wa mkopo
2.	Ufadhili wa elimu ya juu kutoka taasisi na watu binafsi	- Hupunguza utegemezi wa kifedha kwa mwanafunzi na familia. - Huongeza fursa ya kuendelea na masomo. - Mara nyingi hauhitaji kurejeshwa.	- Ushindani mkubwa wa kupata ufadhili. - Baadhi ya wafadhili huweka masharti maalumu.
3.	Akiba mbalimbali	- Hutoa uhuru wa kifedha. - Husaidia kukabiliana na dharura.	- Inaweza isiwe ya kutosha kugharimia mahitaji yote.
4.	Faida itokanayo na uwekezaji mbalimbali	- Huongeza kipato bila kutegemea ajira. - Hujenga utajiri wa muda mrefu. - Inajenga msingi wa uwekezaji kwa vizazi (generational wealth).	- Kuna hatari ya kupata hasara, hivyo unahitaji kuwa na uwekezaji zaidi ya mmoja kukabiliana na hasara. - Inahitaji mtaji wa kuanzia. - Baadhi ya uwekezaji huhitaji muda mrefu kabla ya kupata faida hivyo, inahitaji uvumilivu.
5.	Fedha za kujikimu kutoka kwa wazazi	- Hupatikana kwa urahisi kwa wanafunzi wengi. - Humpa mwanafunzi muda wa kuzingatia masomo. - Hakuna deni la kulipa.	- Huongeza utegemezi kwa wazazi. - Wazazi wanaweza kushindwa kutoa fedha kwa wakati.

S/N	Chanzo	Faida	Hasara
6.	Biashara mbalimbali	- Huzalisha kipato cha ziada. - Hujenga ujuzi wa ujasiria-mali. - Inaweza kukua na kuwa chanzo kikubwa cha mapato baada ya kuhitimu.	- Inaweza kuathiri muda wa masomo endapo hakuna mpangilio na matumizi sahihi ya muda. - Inahitaji mtaji wa kuanzia. - Kuna uwezekano wa - kupata hasara za biashara.
7.	Kazi za muda mfupi (Part-time jobs)	- Hutoa kipato cha kujikimu. - Hujenga uzoefu wa kazi. - Husaidia kujifunza nidhamu na uwajibikaji.	- Inaweza kuathiri muda wa masomo endapo hakuna mpangilio na matumizi sahihi ya muda. - Kipato kinaweza kuwa kidogo. - Huongeza uchovu na msongo wa mawazo.
8.	Mafunzo ya kazi (Intern-ship)	- Hutoa uzoefu wa kazi unao-hitajika sokoni. - Baadhi ya taasisi hutoa posho. - Huongeza nafasi za kupata ajira baada ya kuhitimu.	- Si taasisi zote zinazotoa po-sho. - Posho ya kazi inaweza kuwa ndogo. - Wakati mwingine kazi zinazo-fanywa haziendani na matara-jio ya mwanafunzi.

2.7.4 Njia za Kufanya Biashara

Biashara zinaweza kufanyika kwa njia kuu mbili, ambazo ni biashara za kawaida (traditional businesses) na biashara za mtandaoni (online businesses). Kila njia ina faida na hasara zake kama ifuatavyo:

S/n	Aina ya Biashara	Faida	Hasara
	Biashara za kawaida (traditional businesses)	- Wateja wanaweza kuona na kukagua bidhaa kabla ya kununua. - Huongeza uaminifu kati ya muuzaji na mteja kwa sababu ya mawasiliano ya moja kwa moja - Rahisi kuwahudumia wateja ambao hawatumii teknolojia. Malipo yanaweza kufanyika papo hapo.	- Inahitaji mtaji mkubwa wa kupanga au kujenga eneo la biashara. - Gharama za uendeshaji ni kubwa (kodi ya pango, umeme, maji, n.k.). - Wateja hupatikana zaidi katika eneo husika tu. - Biashara husimama wakati duka limefungwa.
	Biashara za mtandaoni (online businesses)	- Hufikia wateja wengi kwa wakati mmoja. - Gharama za kuanzisha ni ndogo kuliko biashara ya kawaida. - Biashara inaweza kufanya kazi saa 24 kwa siku. - Hutoa urahisi wa kufanya kazi ukiwa popote.	- Nahitaji ujuzi wa teknolojia na matumizi ya mtandao. - Kuna hatari ya utapeli wa mtandaoni. - Baadhi ya wateja hawawezi kuamini bidhaa kabla ya kuiona. - Changamoto za usafirishaji na ucheleweshaji wa bidhaa. - Inategemea upatikanaji wa intaneti na umeme.

2.7.5 Hitimisho

Kila chanzo cha kipato kina faida na changamoto zake. Kama mwanafunzi unapaswa kuchagua chanzo kinachoendana na uwezo wako, muda ulionao, na malengo yako ya masomo ili kuhakikisha kuwa kipato kinapatikana bila kuathiri mafanikio yako kitaaluma.

Maswali

1. Nini maana ya kipato?
    a. Pesa anazopata mtu kutoka kwa wazazi wake tu.
    b. Fedha au rasilimali anayopata mtu, familia au taasisi kutokana na kazi, biashara, au uwekezaji
    c. Mkopo unaotolewa na serikali kwa wanafunzi
    d. Akiba inayowekwa benki kwa matumizi ya baadaye
2. Ni ipi kati ya hizi ni umuhimu wa kipato?
    a. Pesa anazopata mtu kutoka kwa wazazi wake tu.
    b. Kufanikisha malengo ya maisha kama kununua nyumba au gari
    c. Kuongeza utegemezi kwa wengine
    d. Kupunguza fursa za kupata elimu
3. Ni chanzo kipi cha kipato ambacho hakihitaji kulipwa baada ya kuhitimu?
    a. Mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
    b. Kazi za muda mfupi (part-time jobs)
    c. Ufadhili kutoka kwa taasisi na watu binafsi
    d. Mkopo kutoka benki
4. Ni hasara ipi kuu ya kupata fedha za kujikimu kutoka kwa wazazi?
    a. Hutoa elimu nzuri kwa mwanafunzi
    b. Huongeza utegemezi kwa wazazi na wanaweza kushindwa kutoa kwa wakati
    c. Hupunguza muda wa masomo
    d. Haipatikani kwa wanafunzi wengi
5. Ni chanzo kipi cha kipato kinachoweza kukua na kuwa chanzo kikubwa cha mapato baada ya kuhitimu?
    a. Mkopo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
    b. Fedha za wazazi
    c. Biashara mbalimbali
    d. Mafunzo ya kazi (internship)
6. Ni hasara ipi kuu ya uwekezaji kama chanzo cha kipato?
    a. Huzalishi kipato chochote
    b. Huhitaji mtaji wa kuanzia na kuna hatari ya kupata hasara
    c. Unahitaji elimu ya chuo pekee
    d. Unafanyika nje ya Tanzania tu

2.8 Kujitegemea



Kujitegemea ni uwezo wa mtu kujiamini na kutegemea nguvu zake mwenyewe bila kuhitaji msaada wa watu wengine kila wakati. Kujitegemea ni pamoja na nyanja zifuatazo;


i. **Kiuchumi**: kupata kipato chako mwenyewe na kukidhi mahitaji yako bila kuomba pengine.

ii. **Kifikra**: kufanya maamuzi yako mwenyewe bila kusukumwa na wengine.

iii. **Kihisia**: kudhibiti hisia zako na kuwa imara bila kutegemea faraja ya wengine kila wakati.

iv. **Kijamii**: kuishi maisha yako bila kuwa tegemezi kwa familia au jamii.

Mfano: Mwanafunzi anayejitegemea ni yule ambaye badala ya kusubiri pesa za wazazi tu, anaendesha biashara ndogo, au anafanya kazi ya muda mfupi.



Kama mwanafunzi, unapomaliza chuo safari mpya ya kujitegemea inaanza inakuhitaji kuwa na utayari, ujasiri wa kuchukua hatua ili kuweza kujitegemea. Kuna njia mbili za kujitegemea baada ya kuhitimu masomo, ama kujiari au kuajiriwa. Kuajiriwa ni njia ya moja kwa moja baada ya kuhitimu. Kwa upande wa pili, kujiajiri kunahitaji ubunifu na mtaji. Mtaji unaweza kupatikana kupitia akiba, hii inaweza isijitosheleze. Fursa nyingine zinapatikana kupitia mifuko ya fedha ya kiserikali inayotoa fursa kwa vijana kupitia vikundi.

2.8.1 Faida na Hasara za Njia za Kijiajiri na Kuajiriwa

S/n	Njia za Kujitegemea	Faida	Hasara
1.	Kujiajiri	- Uhuru wa kupanga muda wako wa kazi. - Kipato kinaweza kuwa kikub-wa kulingana na juhudi zako na fursa za kukuza biashara. - Unakuwa mmiliki wa biashara yako mwenyewe na uwezo wa kufanya maamuzi bila kushurutishwa.	- Kipato si cha uhakika (kinaweza kupanda au kushuka). - Hatari ya hasara ya biashara. - Unawajibika mwenyewe kwa mafanikio na kushindwa. - Changamoto za kupata mtaji. - Msongo wa mawazo kutokana na majukumu mengi.
2.	Kuajiriwa	-Kipato cha uhakika (mshahara wa kila mwezi). -Usalama zaidi wa kifedha na kijamii. -Faida kama bima ya afya, pen-sheni, likizo. -Majukumu ni maalum na yanaelekezwa.	- Uhuru mdogo wa kufanya maamuzi. - Kipato kina kikomo (kuna kustaafu au kuachishwa / kupoteza ajira). - Unafuata sheria na ratiba za mwajiri. - Fursa ndogo ya kujitengenezea utajiri mkubwa.

Mfano: Kujiajiri Baada ya Chuo

Mhitimu ameanzisha biashara ndogo kwa mtaji wa Sh. 2,000,000. Katika mwezi mmoja mauzo Sh. 1,500,000 na gharama za uendeshaji wa biashara = Sh. 1,000,000.

Swali: Faida ya biashara ni kiasi gani?

Jibu: Faida = Mauzo − Gharama

$$Faida = Mauzo - Gharama$$

$$= 1{,}500{,}000 - 1{,}000{,}000$$

$$= 500{,}000$$

Biashara imetoa faida ya Sh. 500,000 kwa mwezi. Ikiwa faida hii itaendelea kwa miezi 12, mjasiriamali anaweza kupata:

$$500{,}000 \times 12 = 6{,}000{,}000$$

Hivyo, anaweza kupata Sh. 6,000,000 kwa mwaka, jambo linaloonesha jinsi kujiajiri kunavyoweza kuongeza kipato.

2.82 Namna ya Kujilinda na Hasara za Kuajiriwa na Kujiajiri

S/n	Chanzo	Namna ya Kujilinda
1.	Kujiajiri	- Kufanya utafiti wa soko kabla ya kuanzisha biashara ili kuelewa mahitaji ya wateja. - Kuwa na mpango mzuri wa biashara (business plan) unaoelekeza matumizi na mapato. Kuweka akiba na mtaji wa dharura kwa ajili ya nyakati za biashara kuwa chini. - Kuchukua bima ya biashara ili kulinda mali na bidhaa dhidi ya majanga. - Kudhibiti matumizi na kutumia fedha kwa uangalifu ili kuepuka hasara zisizo za lazima. - Kujifunza ujuzi wa usimamizi wa biashara na masoko ili kuongeza ushindani. Kutofautisha matumizi binafsi na gharama za biashara.

2.	Kuajiriwa	- Kuweka akiba ya mara kwa mara ili kuwa na hifadhi ya dharura endapo ajira itakoma. - Kujifunza na kuongeza ujuzi (Upskilling / skills upgrading) ili kuongeza thamani kazini na kupunguza hatari ya kuachishwa ajira. - Kuwekeza vyanzo vingine vya kipato kama biashara ndogo au uwekezaji. - Kuwa na bima ya afya na bima nyingine muhimu ili kupunguza mzigo wa gharama zisizotarajiwa. - Kujenga mtandao wa kitaaluma (professional networking) ili kupata fursa mpya za kazi kwa urahisi.

2.8.3 Hitimisho

Uchaguzi kati ya kujiajiri na kuajiriwa unategemea malengo, ujuzi, na mazingira ya mtu binafsi. Hata hivyo, mchanganyiko wa njia zote mbili unaweza kuwa suluhisho bora kwa kukuza usalama wa kifedha, kujitegema na maendeleo endelevu ya kiuchumi.

Wewe Ndo Future, Timiza Wajibu wako!

Maswali

1. Nini maana ya kujitegemea kifikira?
    a. Kutumia akili ya wengine kufanya maamuzi
    b. Kufanya maamuzi yako mwenyewe bila kusukumwa na wengine
    c. Kuiga maamuzi ya watu wengine
    d. Kuomba ushauri wa daktari kila wakati
2. Ni faida zipi mbili kuu za kujiajiri?
    a. Mshahara wa uhakika na likizo za malipo
    b. Uhuru wa kupanga muda wa kazi na kipato kinaweza kuwa kikubwa kulingana na juhudi
    c. Bima ya afya na pensheni
    d. Uhuru mdogo na majukumu maalum
3. Ili kujilinda na hasara za kujiajiri, nini cha kwanza kufanya kabla ya kuanzisha biashara?
    a. Kukopa pesa nyingi benki
    b. Kufanya utafiti wa soko ili kuelewa mahitaji ya wateja
    c. Kuacha masomo na kufanya biashara
    d. Kuomba msaada wa marafiki
4. Mtu anayeajiriwa anashauriwa kujilinda vipi dhidi ya hatari ya kupoteza kazi?
    a. Kuomba mwajiri mshahara mkubwa kila mwezi
    b. Kuweka akiba ya mara kwa mara, kuongeza ujuzi (upskilling), na kuwekeza vyanzo vingine vya kipato
    c. Kukaa nyumbani na kusubiri kazi nyingine
    d. Kuomba mkopo wa dharura benki

3. Marejeo

1. Bodie, Z., Kane, A., & Marcus, A. J. (2024). Personal Finance (3rd ed.). New York: McGraw-Hill Education.

2. Clason, G. S. (2019). The Richest Man in Babylon. New York: Signet Classics.

3. Collins, J. L. (2016). The Simple Path to Wealth: Your Road Map to Financial Independence and a Rich, Free Life. California: CreateSpace Independent Publishing.

4. Higher Education Students' Loans Board (HESLB). (2024). Loans Issuance and Repayment Guidelines. Dodoma, Tanzania: HESLB.

5. Morgan Housel. (2020). The Psychology of Money: Timeless Lessons on Wealth, Greed, and Happiness. Hampshire: Harriman House.

6. National Financial Education Council (NFEC). (2023). Financial Literacy Standards and Benchmarks. Washington, DC: NFEC.

7. Reserve Bank of Australia. (2021). Financial Literacy and Money Management Guide for Students. Sydney: Reserve Bank of Australia.

8. Trench, W., & Harrison, T. (2021). Managing Personal Finances for Young Adults and Students. London: Routledge.

9. Save and Spend: An E-Book for College Students (2023). Universiti Technology Mara, Malaysia.

10. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) (2021). Misingi ya Elimu ya Fedha na Ujasiriamali.

11. Benki kuu ya Tanzania (2023). Mtaala wa Waelimishaji Waliothibitishwa wa Elimu Ya Fedha.

12. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Na Dhamana .Mtanzania Jihadhari na Upatu Haramu "Ni Hatari kwa Maendeleo Yako na Taifa kwa Ujumla.